Toleo Maalum

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Januari 24, 2022



"Ni wakati sasa wa kuzionesha na kutangaza tamaduni zetu nzuri ili dunia izijue na kuja kuziona."

# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## RAIS SAMIA AUPAISHA UTAMADUNI WA TANZANIA DUNIANI

"Maono na Kampeni kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuufanya utamaduni wa Mtanzania kuwa utalii yamezidi kushika kasi baada ya kuzindua tamasha kubwa la kihistoria la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro, Januari 22, 2022 kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Rais Samia ametoa maelekezo mahususi wa kutaka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuuenzi na kuutangaza utamaduni wa Taifa letu.

Amekwenda mbali zaidi kwa kutangaza kuwa atakuwa Mwenyekiti wa jukwaa la machifu nchini ili kuweza kushirikiana kikamilifu katika kuenzi utamaduni wa taifa letu.

Tunapenda kumpongeza Mhe. Rais kwa mikakati hiyo yenye lengo la kutumia utajiri wa tamaduni wetu kutangaza nchi yetu duniani.

Tunatoa wito kwa wadau wote nchini kuunga mkono jitihada hizi zinazofanywa na Rais wetu ili malengo yaweze kutimia kwa faida vizazi vya sasa na baadaye.

**Mhariri**
John Mapepele

**BODI YA WAHARIRI**

**Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**
Dkt. Hassan Abbasi

**Mhariri**
John Mapepele

**Waandishi**
Adeladius Makwega
Shamimu Nyaki

**Mpiga Picha**
Joseph Kigingi






# Rais Samia Azindua Tamasha la Kilimanjaro, Asifu Ubunifu wa Wizara, Wadau

Na. Mwandishi wetu

Rais Samia Suluhu Hassan Januari 22, 2022, amezindua Tamasha kubwa la Utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro lililoandaliwa kwa pamoja kati ya Wizara ya Utamaduni, Mkoa wa Kilimanjaro na Machifu wa Mkoa huo.

Katika hotuba yake , Rais Samia, licha ya kusisitiza kuwa mengi yamefanyika tangu Serikali yake ilipoamua kuunda Wizara mpya ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, amefafanua kuwa ameteua vijana hodari katika Wizara hiyo ambao wanafanya mageuzi makubwa kwa sasa akitamtaja Waziri Mohammed Mchengerwa, Naibu wake Pauline Gekul, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbasi na Naibu wake Saidi Yakubu.

"Wizara hii sasa imekuwa ya ubunifu na sasa tunaona matamasha mengi yanataribiwa kwa kushirikisha wadau ikiwemo hili la Utamaduni la Kilimanjaro," alisema Rais Samia akiagiza Wizara ya Sanaa na ile ya Utalii kubuni Matamasha mengi zaidi ili kuitangaza nchi kimataifa.

Amesema Baba wa Taifa, Julius Nyerere aliwahi kusema Utamaduni ni kiini na roho ya taifa lolote na kwamba nchi isiyokuwa na utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu wasiokuwa na roho.



# Maonesho ya Vyakula vya Asili Kwenye Tamasha la Kilimanjaro Yafunika

Na. John Mapepele

Maonesho ya vyakula na asili vya makabila vya wamasai, wachaga na wapare kwenye tamasha kubwa la utamaduni la mkoa wa Kilimanjaro lililofanyika kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi yameongeza radha ya tamasha hilo na kuwa kivutio kwa watu wengi waliohudhuria wakiongozwa na Rais Samia.

Makabila yote matatu yalikuwa na mabanda maalum ya maonesho haya ambapo mgeni rasmi katika Tamasha hili Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alikwenda moja kwa moja kupata maelezo ya vyakula hivyo yaliyotolewa na machifu wa kila kabila mara baada ya kuingia uwanjani hapo.

"Nimefurahishwa sana na namna maandalizi ya maonesho haya yalivyoratibiwa" amepongeza Mhe. Rais baada ya kupita na kupata maelezo kutoka kwa machifu hao wa mkoa wa Kilimanjaro.

Maonesho hayo pia yalijumuisha vifaa mbalimbali vya makabila hayo.

Mratibu wa machifu wa mkoa wa Kilimanjaro Joseph Msele amesema umati wa watu uliohudhuria tamasha hilo ulipita kwenye mabanda hayo hali inayoonesha kuwa watu wanapenda vyakula vya asili tofauti na hapo awali.

"Hivi sasa jamii ya watu wetu imeelewa na kuanza kupenda vyakula vya asili kwa sababu ya manufaa makubwa yanayotokana na vyakula vyetu" ameongeza Msele



# Rais Samia Afurahishwa Na Vikundi vya Nyimbo za Asili Kwenye Tamasha La Kilimanjaro

Na SAdeladius Makwega

Vikundi zaidi ya 11 kutoka wilaya zote za mkoa wa Kilimanjaro vinameonesha sanaa za maonesho katika Tamasha la Kilimanjaro lililofanyika jumamosi ya Januari 22, 2022 katika Viwanja vya Chuo cha Ushirika Moshi na kutoa hamasa kubwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Utamaduni Dkt. Emmanuel Temu amesema Wizara kwa kushirikiana na wadau iliamua kushirikisha vikundi hivyo ili kutoa burudani nzuri kwa wananchi.

Aidha, amesema vikundi hivyo viliainishwa na kupatiwa mafunzo maalum ndiyo sababu ya kufanya vizuri katika tamasha hilo. Amekitaja kikundi cha ngoma cha Iringi kuwa kilitoka Wilaya ya Rombo na Kikundi cha Osilgila kilitoka Wilaya ya Sihai.

Kutoka Wilaya ya Same ni Lukanga Sanaa Group, Kutoka Wilaya ya Mwanga ni Kundi la Wazee Nasuro, kikundi cha Lambo daima na pia Kikundi cha Furahisha. Ametaja vikundi vingine ni kikundi Teule. Kutoka Moshi ni kundi la Rosi, Kutoka Wilaya ya Hai kikundi cha utenzi, Kutoka Wilaya Same kuna kikundi cha Gonjanza

Katika hotuba yake, Rais Samia amepongeza kuona watoto wadogo wameshirikishwa ambapo amesema kwa kufanya hivyo wanawarithisha utamaduni.

# Nukuu ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa

"Wizara yetu imeendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wa Sekta ya Utamaduni hususani wazee wa Kimilia na Machifu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa lengo la kuimarisha, kulinda na kuendeleza mila, desturi na Utamaduni wa Mtanzania."



## Nukuu ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul

"Mhe. Rais, umetupa dhamana ya kusimamia Sekta hizi na tunakuahidi tutaendelea kufanya kazi hii kwa ushirikiano, ubunifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha kuwa malengo yako binanfsi, matarajio ya Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na matarajio ya wadau wetu vinafikiwa".



# Nukuu ya Katibu Mkuu wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi

"Utamaduni ni uchumi hivyo vijana wa Tanzania wanatakiwa kuchukua maendeleo chanya ya utamaduni ili kunufaika na kuinua maisha yao na uchumi wa taifa kwa ujumla."



# Nukuu ya naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Saidi Yakubu

"Msingi wa taifa lolote ni utamaduni wake, Taifa lisilo na utamaduni ni taifa lililokufa, sisi kama Wizara tutaendelea kukuza na kuuenzi utamaduni wetu kwa faida ya vizazi vya sasa na baadaye".



# Nukuu ya Mwenyekiti wa Machifu Tanzania na Mwenyekiti wa Machifu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Frank Mareale

"Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe, Samia Suluhu Hassan kwa kuthamini na kushirisha machifu katika kukuza na kulinda utamaduni wa taifa letu."





Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul wakibadilishana mawazo na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dkt. Hassan Abbasi kabla ya kuanza kwa sherehe ya uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul akibadilishana mawazo na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Said Yakubu kabla ya kuanza kwa sherehe ya uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe Pauline Gekul akikagua kikundi cha ngoma za asili cha wamasai mara baada kuwasili kwenye uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na viongozi mbalimbali kwenye jukwaa kuu wakiimba Wimbo wa Taifa kabla ya uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Kilimanjaro, Frank Mareale akimkabidhi Mkuki, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe, Samia Suluhu Hassan ikiwa ni ishara ya kumkaribisha kwenye uzinduzi wa tamasha la Utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan mara baada ya kuvalishwa mavazi rasmi ya uchifu, ngao na mkuki ikiwa ni ishara ya kumkaribisha kwenye uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.





Chifu Mkuu wa Tanzania na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan (aliyekaa) kwenye picha ya pamoja na machifu wa mikoa mbalimbali waliohudhuria uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Umati wa watu waliohudhuria uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul akimkaribisha Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ili aongee na wananchi kwenye uzinduzi wa tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Chifu Mkuu akiwahutubia wananchi waliohudhuria uzinduzi wa tamasha la kwanza la kwanza la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro.









Vikundi kutoka wilaya za mkoa wa Kilimanjaro vikionesha sanaa za maonesho katika Tamasha la Kilimanjaro.



Maonesho ya vyakula na asili vya makabila vya wamasai, wachaga na wapare kwenye tamasha kubwa la utamaduni la mkoa wa Kilimanjaro lililifanyika kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Kilimanjaro.

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU

**Mawasiliano**
P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz